# KISWAHILI

# KISWAHILI  GREDI YA SABA

**KUSIKILIZA NA KUJIBU**

Vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mazungumzo

- Kusikiliza kwa makini
- Kumtazama mzungumzaji
- Kutikisa kichwa
- Kutumia vihisishi
- Kuepuka vizuizi vya mawasiliano

Vipengele vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo

- Kutumia lugha ya adabu
- Kutomkata mzungumzaji anapozungumza
- Ubadilishanaji zamu ufaao
- Kujibu kwa kujikita katika kiini Cha swali

**MSAMIATI WA UFAHAMU**

Eleza maana ya maneno yafuatayo

**Kujinadhifisha**- Ina maana sawa na kujing'arisha _ Hali ya kujisafisha uwe msafi

**Taharuki –** kuwa na hamu ya kutaka kujua kitu kitakachotokea baadaye

**Kitana-** kifaa Cha kuchana nywele

**Wakanawa-** ni kuosha mikono kwa kutumia maji

**Kudadisiwa-** peleleza jambo kwa kuulizauliza maswali

**Eleza maana ya vifungu vifuatavyo**

**Msafiri ni aliye bandarini-** Ina maana mambo kuwa tayari kwa jambo Fulani

**Siku njema huonekana asubuhi –** Ina maana kuwa kufanikiwa kwa jambo Fulani huonekana mwanzoni.

**Mguu niponye-** kukimbia mbio sana ili kujinusuru

**Kuwa na moyo wa simba-** ni kuwa jasiri

**Kuangua kucha-** ni kukata kucha-

**VIAKIFISHI**

**Herufi kubwa**

Herufi kubwa hutumika:

1. Mwanzoni mwa sentensi- mf. Mimi ni mwaafunzi
2. Kuandika nomino za pekee- mf.Tanzania,Africa,Alhamisi,James

**Kikomo**

Kikomo hutumika:

1. Mwishoni mwa sentensi- mf. Mama anapika.
2. Katika ufupisho wa maneno- mf. S. L. P
3. Kuandika tarehe- 22.2.2022
4. Kuandika saa-mf. 10.30
5. Kuandika idadi ya pesa- mf. Shilingi 300.50

**SARUFI**

**Nomino za pekee-**

Nomino za pekee hutumika kutaja majina halisi kama vile:

1. Watu- Njeri, Ongeri
2. Siku- Alhamisi,Jumatatu
3. Nchi- Kenya,Uganda, Tanzania
4. Miezi- Januari,Agosti
5. Mungu,Yesu
6. Mito- L. Baringo, L. Bogoria
7. Milima- Kilimanjaro,Evaresti
8. Miji- Eldoret, Nairobi, Mombasa
9. Sikukuu- Madaraka,Mashujaa

**Nomino za kawaida**

Nomino za kwaida ni majina ya vitu vya kawaida kama vile uwanja, ng'ombe,watu,darasa mtoto, kitabu, daktari mpira na mengine mengi.

**Zoezi**

Orodhesha nomino za pekee na nomino za kawaida kutoka mwenye maneno yafuatayo

Mtu, baiskeli,mvulana,Mola,RwandaEvaresti,Lamu,simu,kadhi,nywele,sinema,bahari,Ijumaa,February,bwawa, mswaki,Kipchoge

**Sauti dh na th katika silabi na maneno**

dha, dhe,dhi,dhi,dhu

tha, the,this,tho,thu

**Maneno yenye sauti dh na th**

Dhamani thamani

Adhiri. Athiri

Dhibiti. Thibiti

**Matumizi ya maneno yenye sauti dh na th katika sentensi**

a) Thamani. Dhamini

Thamani ya nyumba Ile ni kubwa sana

Nadhamini rafiki yangu sana

b) Thelathini. Themanini

Mama alinipa shilingi thelathini ya kununua nyanya

Kitabu hicho kinauzwa shilingi themanini

c) Dhahabu. Thawabu

Mkufu wake ni WA dhahabu

Ukimtendea mtu meme,mungu atakupa thawabu

d) Wadhifa. Dhifa

Mtu yule anawadhifa mkuu serikalini

Tulifanya dhifa kumkaribisha mgeni wetu nyumbani

e) Theluji. Themometa

Mvua ilinyesha kukajaa theluji

Daktari alitumia themometa kupima joto mwilini

**Barua ya kirafiki ya mwaliko**

<u>Mambo ya kuzingatia katika kuandika barua ya kirafiki</u>

1. **Anwani yako.** Andika anwani yako upande wa juu wa mkono wa kulia

   Mf. S.L.P 1296

   NAKURU

2. **Tarehe.** Andika tarehe chini ya anwani yako
3. **Mtajo.** Andika mtu unaeashiria kupokea ujumbe wa barua hio. Mf. Kwa dada mpendwa
4. **Maamkuzi.** Anza barua yako kwa kumwamkua unayemwandia baruaile. Mf pokea salamu nyingi kutoka kwangu
5. **Lugha ya adabu.** Tumia lugha ya adabu k.v tafadhali,nakusihi,natumaini
6. **SARUFI sahihi.** Tumia maneno ya kiswahili ambayo yanaeleweka vizuri
7. **Hati nadhifu.** Tumia mwandiko mzuri unapoandika barua ya kirafiki ili kumwezesha unaemwandikia kuisoma vizuri
8. **Tamati.** Maliza baua kwa kutamatisha ujumbe ulikuwa nayo na pia umwarofu kama mngekutana hivi karibuni
9. **Jina lako.** Andika kiashiria chako mf. Mimi dada yako mpendwa, wako meaminifu. Kisha andika jina lako.

Mfano wa barua ya kirafiki

...na mwenzako, soma barua ya kirafiki ifuatayo.

S.L.P. 98 -10100,
MUTHINGA.
22.12.2022

Kwa dada yangu mpendwa,

Pokea salamu nyingi kama mchanga wa baharini kutoka kwangu. Dada yetu Pendo, mama na baba wote wanakusalimu na kuzidi kukuombea mema.

Je, u hali gani? Ni matumaini yangu kuwa u mzima kama kigongo. Sisi huku nyumbani tunashukuru kuwa hatujambo. Dada Pendo anaendelea vizuri masomoni. Mwaka ujao ataingia Gredi ya Sita. Dada amejifunza mengi shuleni. Hivi sasa anaweza kusimulia hadithi mbalimbali na kuandika visa vya kuvutia. Huwa anafua nguo zake mwenyewe. Mama humsaidia tu kuzipiga pasi. Mama na baba wanaendelea na kazi zao za ukulima. Msimu huu mvua ilinyesha vizuri na mazao yanaendelea kunawiri shambani. Tunatarajia mavuno kochokocho.

Lengo la kukuandikia barua hii ni kukujulia hali na vilevile kukualika kwenye sherehe ya kuadhimisha siku yangu ya kuzaliwa. Sherehe yenyewe itakuwa tarehe 2.1. 2023. Itaandaliwa jioni baada ya shughuli za siku.

Siku hiyo tumepanga kuwa na dhifa murua. Tumeamua kuwa tutaandaa matunda mbalimbali kama matufaha, maparachichi, matikitimaji na ndizi. Hali kadhalika, kutakuwepo na samaki, nyama, maharagwe, njugu na pojo. Isitoshe, ugali, wali, viazi na chapati vitakuwepo kwa wingi. Vinywaji kama maji na sharubati pia vitakuwepo kwa wingi.

Dada, nakuomba ukubali kuongoza shughuli ya ukataji keki siku hiyo. Tafadhali usikose kufika ili tuonane, tujumuike pamoja na tufurahie siku hii muhimu.

Nilitaka upate barua hii haraka iwezekanavyo. Baba ameniruhusu kutumia simu yake. Nimeipiga picha barua hii nikakutumia kwa mtandao wa 'WhatsApp' badala ya kuituma kwa posta. Nitafurahi iwapo utaweza kunijibu kwa njia ii hii kupitia simu ya baba.

Ni mimi ndugu yako mpendwa,
Karani Karamu.

## AINA ZA NOMINO

### Nomino za makundi

Nomino za makundi hutaja vitu vingi vilivyo pamojakama kitu kimoja. Vitu hivo hujitokeza katika kundi au fungu. Mifano ni:

- Fungu la maembe
- Bunda la noti
- Shada la maua
- Thurea ya nyota
- Change la ndizi
- Shehena ya mizigo
- Baraza la wazee
- Mtumba wa nguo
- Msitu wa miti
- Mlolongo wa magari
- Umati wa watu
- Mkungu wa ndizi
- Tita la Kuni
- Genge la majambazi
- Kicha Cha mboga
- Mkururo wa siafu
- Baraza la mawaziri
- Bodies la wasimamizi
- Biwi la takataka
- Shungi la nywele

### Nomino za dhania

Nomino za dhania ni majina ya vitu visivyoweza kuonekana au kushikika kwa mikono. Ni majina ya vitu ambavyo ni vya Kufikiria tu. Mifano ni :

Usingizi. Utandawazi. Furaha

Wema. Shibe. Ualimu

Elimi. Marndeleo. Maisha

Huzuni. Mapema zi. Njaa

Chagua nomino dhania kati ya haya maneno

Kiu,upole,wayo,utamu,bumba,chumba,manukato,Raha,kikosi, ugonjwa

**TANZU ZA FASIHI**

Fasihi ni kazi inayotumia lugha na ishara kwa ubunifu ili kuwasilisha ujumbe kwa Jamii.

Fasihi ikisimuliwa hutwa **fasihi simulizi**

Fasihi ikiandikwa huitwa **fasihi andishi**

Tanzu za fasihi ni mbili

- Fasihi simulizi
- Fasihi andishi

**Sifa za tanzu za fasihi**

<u>Sifa za fasihi andishi</u>

- Hupitishwa kwa njia ya maandashi
- Ni Mali ya mtu binafsi
- Haiwezi kubadilishwa
- Hutumia mbinu za lugha na mbinu za sanaa

<u>Sifa za fasihi simulizi</u>

- Hupitishwa kwa njia ya mdomo
- Ufanisi wa Sanaa katika fasihi simulizi hutegemea uwezo wa msimulizi au wahusika
- Masimulizi yakeyanaweza kuathiriwa na mazingira,hisia na Hali
- Ni Mali ya Jamii. Hakuna mtu Fulani anayemiliki Sanaa katika fasihi simulizi
- Inaweza kubadilika kutoka kizazi Hadi kizazi,au mazingira mbali mbali kwa sababu hutegemea kumbukumbu ya msimulizi
- Angalabu Huwa na funzo Fulani

**Tofauti kati ya hadithi ya kusoma na hadithi ya kusimuliwa**

**Fasihi ya kusimuliwa**

Tofauti kati ya Fasihi Andishi na

FASIHI SIMULIZI

1. Huwasilishwa kwa njia ya mdomo na/au matendo.
2. Ni mali ya jamii.
3. Msimulizi anaweza kubadilisha sehemu fulani
4. Huhifadhiwa akilini
5. Kazi simulizi hubadilika na wakati
6. Huhitaji msimulizi na hadhira yake wawe mahali pamoja wakati wa masimulizi
7. Mtu yeyote anaweza kutunga na kusimulia
8. Hutumia wahusika changamano (wanyama, watu, mazimwi n.k)

**Fasihi ya kusoma**

FASIHI ANDISHI

Huwasilishwa kwa njia ya maandishi

Kazi andishi ni mali ya mwandishi (na mchapishaji)

ni Kitabu kilichoandikwa hakiwezi kubadilishwa

Huhifadhiwa vitabuni

Kazi andishi haibadiliki na wakati

Msomaji anaweza kusoma kitabu cha hadithi peke yake, mahali popote, wakati wowote

Ni lazima mwandishi na msomaji wawe na uwezo wa kusoma

Hutumia wahusika wanadamu.

**AINA ZA tungo za fasihi simulizi na fasihi andishi**

Kuna tanzu nne kuu za Fasihi Simulizi:

1. Hadithi Fupi - kazi andishi ya fasihi isiyokuwa ndefu sana
2. Riwaya - kazi andishi ya fasihi ambayo huwa ndefu kuliko hadithi fupi
3. Tamthilia- kazi andishi ya fasihi inayowasilisha mchezo wa kuigiza
4. Mashairi - mashairi yaliyochapishwa huwa chini ya fasihi andishi.

**Aina za tungo za fasihi andishi ni**

**Aina za tungo za fasihi simulizi ni:**

**VIPERA VYA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI**

| | |
|---|---|
| **HADITHI / NGANO** | • Khurafa<br>• Hekaya<br>• Mighani / Visakale<br>• Usuli / Visaviini<br>• Visasili<br>• Hadithi za Mtanziko<br>• Hadithi za Mazimwi |
| **NYIMBO** | • Mashairi<br>• Kimai<br>• Wawe/Hodiya<br>• Nyimbo za Ndoa<br>• Nyimbo za Kidini<br>• Nyimbo za Kisiasa<br>• Za Tohara/Jandoni<br>• Nyimbo za Kizalendo |
| **TUNGO FUPI** | • Methali<br>• Vitendawili<br>• Mafumbo<br>• Vitanza Ndimi na Vichezea Maneno<br>• Semi<br>• Lakabu<br>• Misimu |
| **MAIGIZO** | • Michezo ya Kuigiza<br>• Ngomezi<br>• Miviga<br>• Malumbano ya Utani<br>• Mazungumzo/Soga<br>• Ulumbi<br>• Vichekesho<br>• Maonyesho |

**NOVELA**

NOVELA ni maandishi ya nathari yaliyo na ploti ya moja kwa moja na wahusika wake Huwa wachache

Mfano wa novela:

# Kovu la Huba



Nana Ayana

# KOVU LA HUBA

Kovu la huba ni novela inayosimulia kisa cha binti anayefiwa na mamake mzazi akiwa kikembe. Sidi anaishia mikononi mwa malimwengu. Anapata hela za kurudi tena masomoni kwa njia ya mtandao. Anasomea shahada ya uanahabari. Akiwa huko kazini, anapendana na Baraka mtoto wa mwajiri wake. Baraka pia ni mwanafunzi wa chuo kikuu. Sidi anapata mimba ya Baraka. Wanachumbiana. Katika pilkapilka hizo, Mzee Solomoni ambaye ni Baba yake Baraka, anajaribu kumshawishi Sidi kufanya mapenzi naye.

Sidi anajithamini. Anakataa vishawishi vya zawadi na pesa. Solomoni anaamua kumbaka Sidi. Kwa bahati mbaya, bastola ambaye mzee huyo amashikia Sidi inafyatuka. Mzee Solomoni anajipiga risasi mwenyewe. Anaanguka na kuzirai. Sidi anakamatwa nakutiwa ndani. Anashtakiwa kwa kosa la jaribio la mauaji. Baraka anamlaani na kumkana. Sidi anapata uchungu wa mimba akiwa kizimbani.

Anajifungua mtoto wa kiume siku hiyo hiyo. Anamwita Johari. Hadithi inapelekea kwisha, ukweli unadhihirika. Solomoni ndiye mwenye makosa. Je Sidi atamfungulia mashtaka Mzee Solomoni ambaye sasa ni babu ya Johari?

**INSHA YA KUBUNI**

Mambo muhimu ya kuzingatia unapoandika insha ya KUBUNI ni:

1. Mada na ujumbe wa kuandikia insha ya kubuni_ jadili na wenzako kuhusu mada na ujumbe mtakao andika.
2. Vidokezo kulingana na mada ya kuandikia insha ya KUBUNI _ vidokezo vinavyolingana na mada mliochagua
3. Vidokezo vyenye ujumbe unaolingana na mada ya insha ya KUBUNI _ andika daftarini vidokezo vya insha ya KUBUNI ulioichagua . Panga vidokezo hivo kwa mtiririko unaofaa
4. Kuandika insha ya KUBUNI _ tumia vidokezo ulivyoipanga kuandika insha ya KUBUNI. Wasilisha insha yako kwa mwalimu asahihishe.

**AINA ZA NOMINO**

**Nomino za wingi na nomino za vitenzi jina**

<u>Nomino za wingi</u>

Nomino za wingi ni maneno ambayo hayabadiliki katika umoja au wingi.

Mifano za nomino za wingi ni:

- Mvua
- Chumvi
- Mate
- Mchanga
- UNGA
- Asali
- Vumbi
- Samli
- Wali
- Maziwa

**Nomino za vitenzi jina**

Nomino za vitenzi jina ni aina za vitenzi ambapo vitenzi mzizi hutiwa kiambishi awali ku- Hutumiwa katika WAKATI uliopita na ujao. Hata hivyo maana ya kitenzi jina Huwa ni sawa na kitenzi jina chake.

Mifano za nomino za vitenzi jina ni:

- Kutunza
- Kuchoka
- Kutetea
- Kupumzika
- Kupona
- Kulishs
- Kupanda
- Kuosha

- Kutibi
- Kusaidia

**Nyimbo za watoto na bembelezi**

Nyimbo za watoto

Nyimbo za watoto ni nyimbo zinazoimbwa a watoto. Nyimbo hizi huimbwa na watoto wanapocheza.

Mfano wa nyimbo za watoto ni:

*Mabata wadogo wadogo x2*
*Wanaogelea x 2*
*Katika ziwa letu la maji safi*
*Wanafanya kwa kwa kwa X2*
*Katika ziwa letu la maji safi.*

*Tumbili wadogo wadogo x2*
*Wanarukaruka x2*
*Katika mitu yetu ya miti ya juu*
*Wanafanya ki ki ki X2*
*Katika mitu yetu ya miti ya juu.*

*Vifaru wadogo wadogo x2*
*Wanatembea x2*
*Wanapanda mlima kwa kwato zao*
*Wanafanya ngwa ngwa ngwa x2*
*Wanapanda mlima kwa kwato zao.*

**Sifa za nyimbo za watoto**

- Huimbwa watoto wanapocheza.
- Nyimbo hizo hurudiwarudiwa.
- Nyimbo hizo huimbwa kwa mahadhi yaani kupandisha na kushukisha sauti.
- Mara nyingi watoto huchezesha mwili wanapoimba

**Bembelezi**

Bembelezi ni nyimbo ambazo huimbwa mtoto ili awache kulia au alale. Bembelezi huimbwa na watoto au watu wazima.

Mfano wa bembelezi

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Mama anakuja lala,*
*Akupe maziwa lala.*

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Baba anakuja lala,*
*Akupenda toto lala.*

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Nyanya anakuja lala,*
*Akuoshe toto lala.*

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Babu anakuja lala,*
*Alete zawadi lala.*

**Sifa za bembelezi**

- Huimbwa kwa sauti nyororo
- Haina urefu kamili
- Maneno katika wimbo huu hurudiwarudiwa
- Huimbwa na watoto au watu wazima
- Mwimbaji hupeleka mwili wake katika Hali ya utulivu na kubembeleza

**KUSOMA KWA UFASAHA**

Mambo muhimu unayohitaji kuzingatia ili kusoma makala kwa UFASAHA:

1. Matamshi bora- yafaa unaposoma makala utamke maneno jinsi inavyostahili
2. Kutumia Kasi ifaayo unaposoma _ hesabu maneno unayoweza kuyasoma kwa muda wa dakika moja.
3. Kutumia sauti ipasavyo unaposoma _ soma makala kwa sauti ili usikike vizuri.
4. KUSOMA kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo_ tumia ishara kama za uso na mikono unaposoma makala.kwa mfano kushukuru,tumia ishara kuonyesha kushukuru

**INSHA YA KUBUNI _ Masimulizi**

**Mambo ya kuzingatia unapoaandika ya masimulizi**

1. Lugha ya kiubunifu katika insha za masimulizi _ tumia methali,nahau,tashbihi na misemo katika insha ya masimulizi.Hii huchangia kuongeza alama kwenye insha yako.
2. Elezea wahusika na mandhari katika insha ya masimulizi _ taja majina Yao,tabia zao,mambo wanayoyafanya,uhusiano wao na maneno wanayosema.
3. Elezea mahali mbalimbali palipotajwa katika insha.

Mfano wa insha ya masimulizi

## MVUMILIVU HULA MBIVU

Ama kweli bidii ni mali. Katika kitongoji cha Sura, paliishi kijana mmoja aliyefahamika kama Kawesa. Kawesa alikuwa katika Gredi ya Saba shule ya Kipepeo. Eneo la Kipepeo lilikumbwa na matatizo kadha wa kadha. Kulikuwa na ukame na ukosefu wa ajira kwa vijana wengi. Kawesa hakufanya ajizi masomoni. Alifahamu fika kuwa ajizi ni nyumba ya njaa. Dhamira yake ikawa kuikomboa jamii yake kutoka katika lindi la umaskini.

Kawesa alikuwa na talanta ya ukimbiaji. Alifanya mazoezi ya mara kwa mara kwenye milima na mabonde. Mwalimu wake wa michezo alimhimiza, "Mtaka cha mvunguni sharti ainame. Ukitia bidii siku moja utakuwa mwanariadha tajika. La muhimu kwa sasa ni kutumia muda wako vizuri katika masomo na michezoni." "Asante sana Bi. Faraja kwa ushauri wako." Kawesa alimwambia.

Kawesa alifuzu na kujiunga na chuo kikuu. Huko, alisomea Elimu ya Mazingira. Pia alijiunga na timu ya wanariadha. Wakati mmoja aliteuliwa kushiriki katika mashindano ya kimataifa ya riadha. Alishinda mbio za nyika. Kawesa alipata tuzo spesheli kwa kuvunja rekodi ya dunia.

Siku ya kurudi nyumbani Kawesa alikaribishwa na wanakijiji katika uwanja wa ndege. Walimwimbia na kumsifu. Alihojiwa na mwanahabari kuhusu tuzo yake. "Je, utaitumia vipi tuzo yako Bwana Kawesa?" "Nataka kuanzisha mradi mkubwa wa maji huko kwetu Kipepeo," Kawesa alimjibu kwa bashasha. Wanakijiji walishangilia na kurukaruka kama ndama.

Ahadi ni deni. Kawesa aliwaleta vijana pamoja na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kushirikiana. Alianzisha mradi wa kuchimba kisima baada ya kupata kibali kutoka kwa maafisa wa mazingira, Wizara ya Maji na Shirika la Ukadiriaji wa Ubora wa Bidhaa. Kisima hicho kiliwafaidi wakazi wa Kipepeo kwa njia tofauti. Walipata maji ya kutumia nyumbani mwao. Wafugaji walipata maji ya mifugo yao. Waliokuza mimea mbalimbali walinyunyizia mashamba yao maji. Vijana nao wakaanzisha mradi wa kupakia na kuuza maji. Eneo la Kipepeo liliimarika sana kimaendeleo. Kweli, kuinamako ndiko kuinukako.

**<u>Zoezi</u>**

Andika insha ya masimulizi inayoanza hivi:

**Ilikuwa yangu ya kwanza kuzuru mbuga ya wanyama. Siku hiyo--------**

**NYAKATI**

**Wakati uliopo**

<u>Vitenzi vilivyo katika WAKATI uliopo</u>

- Ninalima
- Unachimba
- Anatengeneza
- Mnatangaza
- Tunauza

Wakati uliopo huwakilishwana sehemu ya neno **na…** katika neno. Kila neno Lina sehemu ya ..,na…kwenye neno kuonyesha kwamba kitendo kinafanyika WAKATI huo.

**Zoezi**

<u>Pigia mstari  vitenzi katika WAKATI uliopo kwenye kifungu hiki</u>

Eneo la Mokolo linajulikana kwa migodi ya dhahabu. Watu wengi wanafaidika kutokana na biashara ya dhahabu. Hata hivyo, uchimbaji wa migodi ya dhahabu wakati mwingine unahatarisha maisha. Matumizi ya teknolojia ya uchimbaji wa dhahabu yanaweza kuhakikishia wachimbaji migodi usalama wao. Kupanda miti kwa wingi katika eneo la Mokolo kunaimarisha mazingira. Biashara ya dhahabu inaweza kuleta maendeleo makubwa nchini.

**Wakati uliopita**

<u>Vitenzi katika WAKATI uliopita</u>


- Nilinunua
- Walishirikiana
- Walienda
- Walienda

- Alivuna
- Alitanga

Wakati uliopita huwakilishwa na ..,li..katika neno. Mfano ni alilima, kuonyesha kuwa alifanya kitendo hicho na muda umepita tangu afanye kitendo hicho

**Zoezi**

Panga maneno yafuatayo ifaavyo ili kuunda sentensi- sahihi


1. yake kazi Roda mapema alimaliza
2. dhahabu soko katika iliuzwa
3. shuleni jana kitabu alisoma
4. vizuri zilikauka nguo zake
5. ilinyesha mwaka uliopita mvua.

**Wakati ujao**

Maneno katika WAKATI ujao

- Nitapika
- Tutaomba
- Mtashinda
- Atafikiri
- Atasaka

Wakati ujao huwakilishwa na _ ta _ katika neno.

**Zoezi**

Pigia mstari vitenzi katika WAKATI ujao

katika wakati uliopo.

Mgeni mteule atawasili saa sita kamili. Atalakiwa na kundi la wanamazingira. Watapiga foleni mbele ya darasa na kuimba Wimbo wa Taifa. Wanafunzi wengine watashangilia.



**Mazungumzo mahususi**

<u>Mfano wa mazungumzo</u>

*(Ni asubuhi. Bati na Roba wamekutana shuleni nje ya madarasa yao.)*

Bati: Habari ya asubuhi? *(Akimsalimia Roba.)*

Roba: Nzuri. Sijui na wewe? Umeamkaje?

Bati: Sijambo, nashukuru. Leo tutakutana jioni kwa mazoezi ya kukariri shairi?

Roba: *(Kwa uchangamfu)* Bila shaka. Leo lazima tujifunze beti mbili za shairi.

Bati: Sawa basi. Shinda salama. *(Akiingia darasani.)*

Roba: Kwaheri. Tutaonana jioni. *(Akiingia darasa tofauti.)*

*(Baadaye jioni hiyo, Bati na Roba wanakutana ukumbini.)*

Bati: Masalkheri?

Roba: Aheri. Naomba tuanze mazoezi ya kukariri shairi. Muda unatupa kisogo.

Bati: Haya tuanzeni. Beti zenyewe ni nyepesi. Tutazishika haraka.

Maswali:

<u>Maneno ya maamkuzi</u>

<u>Habari</u>

<u>Hujambo</u>

<u>Umeshindaje</u>

<u>Sijambo</u>

Umeamkaje

Shinda salama

Kwaheri

Buriani

Tuonane Tena

Lala salama

Mzuri

Alamsiki

Masalkheri

Aheri

Sabalkheri

Buheri

Habari za asubuhi

Masalkheri

**Majibu ya maamkuzi**

1. Habari ya asubuhi? Njema aunzuri
2. Sabalkheri? Sabalkheri
3. Masalkheri? Aheri/ masalkheri
4. Habari? Njema au mzuri
5. Alamsiki? Binuru
6. Umeshindaje? Vyema
7. Umeamkaje? Vyema/ salama
8. Habari za kutwa? Sina lakuamba au salama
9. Shikamoo? Marahaba
10. Tuonane tene? Inshallah/ mungu akipenda
11. Buheri? Buheri wa afya
12. Buriani? Buriani dawa
13. Lala salama? Pia nawe/ wa salimini
14. Kwaheri? Kwaheri ya kuonana

**INSHA YA maelekezo**

INSHA ya maelekezo ni maelezo ambayo unahitajika kuzingatia katika kutenda shughuli Fulani. Hunuia kueleza waziwazi utaratibu wote na hatuna zote za kufuata katika kutenda jambo Hilo.

**Mpangilio wa hatuna za insha ya maelekezo**

a) Muda wa safari
b) Njia atakayotumia
c) Gari atakaloabiri
d) Vitu atakavyopitia
e) Vitu muhimu atakavyoona

Mfano wa insha ya maelekezo

Jinsi ya kufika KITUO CHA AMANI kutoka Sifa

Fuata maelekezo yafuatayo ili kufika KITUO CHA AMANI kutoka Sifa:

(a) Safari itachukua muda wa karibu saa moja.
(b) Abiri gari nambari 27.
(c) Basi likishaingia katikati ya jiji shuka kwenye kituo cha mabasi cha Leba.
(d) Ukiangalia ng'ambo ya pili ya barabara utaona hoteli kubwa yenye maandishi KULA STAREHE.
(e) Vuka barabara hiyo ili kuelekea upande wa hoteli hiyo.
(f) Kisha fuata barabara inayoitwa FURAHA.
(g) Ifuate hadi pale inapopinda.
(h) Hapo utaona kituo cha Polisi cha LINDA WATU.
(i) Piga kona kushoto ufuate barabara ya RIZIKI.
(j) Endelea nayo hadi ufike barabara pacha (upande wa kushoto).
(k) Vuka barabara hiyo pacha na utakuwa kwenye lango kuu la uwanja wa michezo wa MABINGWA.
(l) Hatua chache, mbele utaona kibao kilichobandikwa maandishi KITUO CHA AMANI kwa rangi nyekundu kushoto.
(m) Tembea kwa mita karibu mia tano utafika kwenye lango kuu la KITUO CHA AMANI.

**Zoezi**

Andika insha ya maelekezo ili kumwelekeza mwenzako Kufikia keenu kutoka shuleni.

**Nyakati na Hali**

**Wakati uliopo Hali ya kuendelea**

Wakati uliopo Hali ya kuendelea huonyesha kuwa kitendo kinaendelea kufanyika Sasa.

Mifano za sentensi zilizo katika WAKATI uliopo Hali ya kuendelea:

1. Mama **anatukaribisha** nyumbani _ kitenzi anatukaribisha kinaonyesha Hali ya kitendo kuendelea
2. Mtetezi wa haki **anazungumza** kuhusu haki za kijinsia
3. Msichana **anakariri** shairi kuhusu usawa katika Jamii
4. Mwanafinzi **anaandika** insha yake
5. Rais wa nchi **anatoa** taarifa sasa

**Zoezi**

Pigia mstari chini ya vitenzi vilivyo katika WAKATI uliopo Hali ya kuendelea kwenye kifungu hiki

Charo anawazungumzia wanakijiji. Anawahimiza kuheshimiana. Anatoa ushauri kwa wote. Anawaomba wanaume na wanawake kushirikiana na kutangamana kwa upendo. Anasema kuwa wasaidiane katika shughuli za maisha ya kila siku.

**Wakati uliopita Hali ya kuendelea**


Wakati uliopita Hali ya kuendelea huonyesha kuwa kitendo kilikuwa kikiendelea WAKATI uliopita.

Mifano za sentensi zilizo katika WAKATI uliopita Hali ya kuendelea

1. Wanafunzi **walikuwa** wakicheza uwanjani
2. Mkulima **alikuwa** alivuna mavuno yake
3. Wakili **alikuwa** akimwakilisha mshtakiwa
4. Wanariadha **walikuwa** wakifanya mazoezi milimani.
5. Msichana **alikuwa** akifurahia KAZI yake

**Zoezi**

Geuza sentensi hizi ziwe katika wakati uliopita Hali ya kuendelea


(a) Nitakapofika dada atakuwa anafyeka nyasi.
(b) Chifu atakuwa akihutubia kuhusu ubora wa mtoto wa kike na wa kiume.
(c) Jamii imekuwa ikipewa mafunzo kuhusu umuhimu wa jinsia zote.
(d) Dagita amekuwa akitia bidii mchezoni.
(e) Haya yamekuwa mawaidha bora.

**Wakati ujao Hali ya kuendelea**

Wakati ujao Hali ya kuendelea huonyesha kuwa kitendo kitakuwa kikiendelea siku za usoni

Mifano za sentensi zilizo katika WAKATI ujao Hali ya kuendelea

(a) Mhudumu atakuwa akiwaelekeza wageni.

(b) Dereva wa kike atakuwa akiendesha gari jipya.

(c) Galgalo atakuwa akiwahamasisha kuhusu tamaduni zilizopitwa na wakati.

(d) Yosi atakuwa akitazama habari kwenye runinga.

(e) Chifu atakuwa akiwatahadharisha dhidi ya ndoa za mapema.

3. Soma kifungu kifuatacho kisha unakili daftarini vitenzi vilivyo katika wakati ujao hali ya kuendelea.

Atieno atakuwa akiwaongoza wenzake darasani kama kiranja. Atakuwa akitarajiwa kuwa kielelezo bora kwa wenzake. Wenzake darasani watakuwa wakimsikiliza. Pia watakuwa wakimpa mapendekezo yao. Atieno atakuwa akiyawasilisha kwa mwalimu wa darasa.

**Martini**

Martini ni kifungu Cha habari kilichoandikwa

Mambo unayozingatia unapofafanua habari unayosikiliz

1. Masuala kuu yanayozungumziwa kwenye martini
2. Habari katika martini
3. Maana ya MSAMIATI ulivyotumika katika martini
4. Kutabiri kitakachotokea katika martini kabla ya KUSIKILIZA

**Maudhui na dhamira**

Maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika KAZI ya fasihi

Dhamira ni lengo la mwandishi kutunga KAZI yake.

Mfano wa novela:

# KOVU LA HUBA

Kovu la huba ni novela inayosimulia kisa cha binti anayefiwa na mamake mzazi akiwa kikembe. Sidi anaishia mikononi mwa malimwengu. Anapata hela za kurudi tena masomoni kwa njia ya mtandao. Anasomea shahada ya uanahabari. Akiwa huko kazini, anapendana na Baraka mtoto wa mwajiri wake. Baraka pia ni mwanafunzi wa chuo kikuu. Sidi anapata mimba ya Baraka. Wanachumbiana. Katika pilkapilka hizo, Mzee Solomoni ambaye ni Baba yake Baraka, anajaribu kumshawishi Sidi kufanya mapenzi naye.

Sidi anajithamini. Anakataa vishawishi vya zawadi na pesa. Solomoni anaamua kumbaka Sidi. Kwa bahati mbaya, bastola ambaye mzee huyo amashikia Sidi inafyatuka. Mzee Solomoni anajipiga risasi mwenyewe. Anaanguka na kuzirai. Sidi anakamatwa nakutiwa ndani. Anashtakiwa kwa kosa la jaribio la mauaji. Baraka anamlaani na kumkana. Sidi anapata uchungu wa mimba akiwa kizimbani.

Anajifungua mtoto wa kiume siku hiyo hiyo. Anamwita Johari. Hadithi inapelekea kwisha, ukweli unadhihirika. Solomoni ndiye mwenye makosa. Je Sidi atamfungulia mashtaka Mzee Solomoni ambaye sasa ni babu ya Johari?

1 234567 890128

**Maudhui yanayojitokeza katika kurasa hii ya novela kovu la huba ni:**

1. **Elimu.** Sidi anapopata Hela za kurudi masomoni,anasomea shahada ya uanahabari
2. **Mapenzi.** Sidi anapendana na baraka ambaya ni mtoto wa mwajiri wake
3. **Ndoa.** Sidi na baraka wanachumbiana baada ya sidi kupata mimba.
4. **Ubakaji.** Solomon ambaye ni babake baraka anajaribu kumbaka sidi

**Dhamira katika novela hii**

Dhamira inayojitokeza katika novela ni uozo katika Jamii kudhulumuwana ukosefu wa haki.

Uozo unajitojeza pale ambapo Solomon anajaribu kumbaka sidi ambaye ni mke wa mwanae .

Sidi pia anadhulumiwa kimapenzi na Solomon ambaye ni baba ya baraka

Pia sidi anadhulumiwa baraka anapomlaani na kumkana

Ukosefu wa haki unajitojeza pale ambapo sidi anashtakiwa kwa kosa la mauji ambalo si la kweli.

**Insha ya masimulizi kutokana na picha**

Viegezo vya kuzingatia wakati wa kuandika insha ya picha

- Tazama picha kwa making Kisha uipe anwani inayooana na kisa Cha picha hizo
- Fikiria kwa making kuhusu ujumbe ambao picha hizo zinaashiria
- Elezea mambo yanayotokea katika kila picha
- Panga na uandike vidokezo vya maelezo ya mambo yanayotokea kwenye picha
- Andika insha ya masimulizi kutokana na vidokezo ulivyoandika

**Aina za vitenzi**

**Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi**

Kitenzi kikuu hupatikana katika sentensi na ndicho hutoa dhana au wazo kuu katika sentensi hiyo. Kitenzi hiki hutangulizwa kwa kitenzi kingine.


Huwa Cha pili katika mfuatano wa vitenzi viwili kwenye sentensi moja.

Mfano ni; mtoto alikuwa akilia kwa sauti ya juu. Neno akilia ndicho kitenzi kikuu

Kitenzi kisaidizi husaidia kitenzi kikuu kufanikisha wazo kuu. Huandamana na kitenzi kikuu kutoa taarifa kamili.

Huwa Cha kwanza katika msururu wa vitenzi. Huchukua viambishi awali vya nafsi,ngeli,WAKATI na Hali. Mfano ni; mtoto alikuwa akilia kwa sauti ya juu. Neno alikuwa ndicho kitenzi kisaidizi.

**Zoezi**



2. (a) Nakili daftarini kifungu kifuatacho:

Marita alitaka kukimbia alipoisikia sauti ya radi. Mwalimu wake alikuwa amesimama karibu na darasa lao. Mwalimu aliweza kumwona. Alimsimamisha. Alitaka kumtuliza ili asiogope sana. Akamwambia, "Marita, umesahau shule yetu ni salama. Tuliwaeleza kuwa imewekwa vidhibiti radi." "Asante mwalimu kwa kunikumbusha. Itabidi niwakumbushe wenzangu."

(b) Pigia mstari vitenzi vikuu katika kifungu ulichonakili daftarini.

(c) Dondoa vitenzi visaidizi na uviandike daftarini.

**KUSIKILIZA kwa UFAHAMU**


Mambo muhimu yanakusaidia kupata ujumbe vizuri unaposokiliza UFAHAMU ni

- Kutazama picha na kueleza unachokiona kwenye picha
- KUJIBU maswali ya UFAHAMU
- Kujadili kifungu Cha UFAHAMU
- Kueleza maana ya MSAMIATI uliopo katika UFAHAMU kutumia kamusi
- Jadili ujumbe unaojitokeza kwenye UFAHAMU

**UFUPISHO**

Habari inaweza kuwasilishwa kwa maneno machache. Hio ndio ufupisho.

Mfano:




## Habari kwa ufupi

(i) Wanafunzi wawasaidia wanakijiji kusafisha Mto Galana.

(ii) Waziri wa Elimu ahimiza ushirikiano kati ya wananchi na uongozi wa shule.

(iii) Walezi washauriwa kuwahimiza watoto wao kudumisha nidhamu.

**<u>Soma kifungu hiki</u>**



1. Soma kifungu hiki.

Elimu barani Afrika imekuwepo kwa miaka na mikaka. Kabla ya majilio ya wamishenari, watoto walipata mafunzo yao nyumbani. Nyanya na babu walikuwa na nafasi kubwa katika kuwaelekeza na kuwafunza watoto. Elimu hii haikuwa imeratibiwa lakini wanajamii walipata mafunzo kuhusu masuala yote ya maisha. Elimu kuhusu kilimo, biashara, dini, uzazi na ndoa ilitolewa.



Hakiuzwi

Aidha, ulikuwa wajibu wa kila mwanajamii kuhakikisha kuwa kuna maadili na nidhamu.

Wamishenari walianzisha shule barani Afrika na kubadili elimu. Elimu ya wamishenari ilichukua mkondo tofauti na ile ya Mwafrika. Elimu ya wamishenari ilikuwa na urasmi na iliendelezwa katika shule. Mwanzoni, ni Waafrika wachache tu waliteuliwa kujiunga na shule hizo.

Elimu ya shule ilimsaidia Mwafrika kugundua hila za mkoloni. Alianzisha harakati za kupigania uhuru. Hatimaye, nchi za Kiafrika zilijikomboa. Ukombozi huu umesaidia nchi za Kiafrika kujitegemea kijamii, kisiasa na kiuchumi. Si hayo tu, elimu imeendelea kuwasaidia wanajamii kutambua na kuheshimu haki zao za kibinadamu.

Elimu ya shule hufungua akili za mtu, kupanua mawazo na mtazamo wake wa maisha. Jamii huwa na sura mpya zipatapo wataalamu na mafundi mbalimbali kama vile walimu, wasusi, wafanyabiashara, mahakimu, wahandisi na wakulima. Elimu hii huwafanya watu kuwa na maono na matarajio mbalimbali ya maisha yao ya baadaye. Elimu huchochea ndoto za watu katika maisha. Ndoto hizi hupandwa na kupaliliwa katika shule kupitia mafunzo, ushauri na vielelezo.

Siku hizi elimu ya shule inapatikana kwa njia nyingi. Njia mojawapo ni ya kiteknolojia. Ujuzi na maarifa mengi yanapatikana katika mitandao rasmi na isiyo rasmi. Mtu anaweza kupata mafunzo na kufuzu kwa njia ya teknolojia ya habari na mawasiliano, yaani TEKNOHAMA.

**Maswali:**

1. Ukiwa na mwenzako andikeni sentensi moja kuhusu kila aya ya kifungu mlichosoma kisha kila mmoja aseme alichoandika.
2. Muombe mwalimu kutoa maoni kuhusu mlivyofupisha aya nzima kwa sentensi moja.

**<u>Fupisha kifungu ulichosoma kwa kuandika sentensi moja kuhusu Kila Aya:</u>**

**INSHA YA KUBUNI _Maelezo**

INSHA ya maelezo ni insha ambayo inatoa taarifa kuhusu jambo au kitu

Mfano wa insha ya maelezo

1. (a)

## KUJIKINGA DHIDI YA UGONJWA WA KORONA

Ugonjwa **hatari** wa korona ni ugonjwa wa **kuambukiza**. Kuna njia mbalimbali za **kujikinga** kutokana na ugonjwa wa korona. Njia mojawapo ni kuvaa maski. Tunashauriwa kuvaa maski safi na inavyostahili. Pia, maski ivuliwe kwa njia inayofaa.

Mtu anaweza kujikinga dhidi ya ugonjwa wa korona kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji **safi** mara kwa mara. Sabuni huua **virusi** vya korona. Kukaa **mbali** na mwenzako ni njia nyingine ya kujikinga kutokana na maradhi ya korona. Wataalam wanahimiza watu kila uchao kukaa umbali wa mita moja na nusu au zaidi hasa wakati wa **mkurupuko** wa ugonjwa huu.

**Chanjo** dhidi ya ugonjwa wa korona imethibitishwa kuwa ni njia mwafaka ya kupambana vilivyo na makali ya korona.

- Unapoandika insha ya maelezo:
  - Tumia MSAMIATI ufaao katika kutoa maelezo
  - Toa maelezo kulingana na mada uliopewa.
  - Tumia MSAMIATI unayoeleweka vizuri,unaoburudisha na unao shawishi.

**SARUFI**

**Aina za vitenzi _ Vitenzi vishirikishi**

Vitenzi vishirikishi ni maneno ambayo hushirikisha mtu au kitu na Hali au tabia Fulani. Mifano ni kama vile: ni,si,yu,ndiye,ndio,,ndipo,ndiko na ndiwo.

2. Mkiwa katika kikundi, tambueni vitenzi vishirikishi vilivyotumika katik sentensi hizi:
   (a) Shule yetu i karibu na kituo cha polisi.
   (b) Pale ndipo pachafu.
   (c) Mwanafunzi angali safarini.
   (d) Tuta hilo ndilo zuri.
   (e) Yeye si mbishi, ni mtiifu wa sheria.
   (f) Ateyo yu mwenye afya.
   (g) Ziwa hili li miongoni mwa rasilimali za nchi yetu.
   (h) Ushirikiano kati ya shule na jamii u wa kiwango cha juu.

**Tunga sentensi ukitumia vitenzi vishirikishi vifuatavyo:**

I) Ni
II) Ndicho
III) H
IV) U
V) I
VI) Yu
VII) Ndiye

**Kuzungumza ili kupasha habari**

Kuzungumza ili kupasha habari ni mazungumzo yanayotoa ujumbe kuhusu kitu,mada au jambo Fulani.

**Aina za kuzungumza ili kupasha habari**

1. Hotuba
2. Majadiliano
3. Mahojiano
4. Mafunzo shuleni
5. Semina
6. Mihadhara

**Vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza ili kupasha habari.**

- Tumia lugha nadhifu
- Kujitambulisha kwa mzungumzaji
- Mada inayozungumziwa ilingane na wasikilizaji
- Kuwapa fursa wasikilizaji kuuliza au kutoa maoni

**Mandhari**

Mandhari ni mazingira au mahali ambapo matukio hutendekea au hutokea.

**Mandhari mbalimbali ya novela**

- Shuleni
- Michezoni
- Kotini
- SoMwituni
- Nyumbani
- Hospitalini

**Umuhimu wa mandhari ya novela**

Mandhari husaidia:

1. Kueleza ujumbe
2. Kukumbuka hadithi
3. Kutambua sifa za wahusika
4. Kukuza hamu ya kuendelea kusoma novela.

**Ploti**

Ploti ni mfuatano wa matukio katika KAZI ya fasihi kama vile novela.

**Mfano**

**Ploti ya novela ulanguzi wa watoto**

- Ulanguzi unahusu kuwateka watoto nyara
- Watoto wawili walikuwa njiani wakitembea Toka sokoni
- Wakamuona mtu wasiyemjua akiwa anawashiria
- Mtu huyo akawafuata akitaka kuwashika
- Watoto walikimbilia kituo Cha polisi ambapo waliokolewa

**VIAKIFISHI**

1. **Kiulizi**

Alama ya kiulizi ni **?**

**Matumizi ya kiulizi**

- Kiulizi hutumika kuuliza mahali,WAKATI, mtendaji au kitendo na kadhalika

**Mifano za sentensi zenye kiulizi (?)**

1. Je, umewahi kusikia kisa Cha ulanguzi wa binadamu?
2. Ulanguzi wa binadamu hutokea wapi?
3. Unaenda wapi?

**Koma**

**Matumizi ya koma:-**

Hutumika

1. Mahali msomaji anapopumua ama anapotua,mf.Nilipokula na kushiba,nilifunganya virago vyangu
2. Tunapoandika anwani, mf. Shule ya Bidii,S.L.P 20040, Nakuru
3. Kutenganisha orodha ya maneno, mf. Alinunua mkate, maziwa,sukari na kahawa.

1. Ambatisha matumizi ya kiakifishi koma na mfano sahihi kwenye chati.

| Matumizi | Sentensi |
|---|---|
| (a) Kuandika mtajo | Sanduku la Posta,<br>0981287,<br>Niru. |
| (b) Kutenga vitu katika orodha | Juma alisema, " Nimefaulu kabisa kuwanasa walanguzi wote." |
| (c) Pumziko fupi | Kwa Mkurugenzi, |
| (d) Kutoa maelezo zaidi | 4,987,521 |
| (e) Kuandika anwani | Tulipogundua ametoweka, tulipiga ripoti kwa polisi. |
| (f) Kuandika tarakimu | Alinunua samaki, nyanya, vitunguu, chumvi na sukari. |
| (g) Katika usemi halisi | Mkuu wa Wilaya, Bi. Sera, amehakikisha watoto wako salama. |

2. Andika sentensi tano kuonyesha matumizi mbalimbali ya koma.

**SARUFI**

**Ngeli ya A__WA**

**Nomino ya ngeli ya A_ WA**

Maneno yafuatayo yako katika ngeli ya A_WA:

Uteo

Sokwe

Nzu

Mto

Mtaro

Vifaranga

Ngano

Ngamia

Chura

Kiangazi

Samaki

Sabuni

Wadudu

Kiota

Mitume

Nyuki

**Viambishi vya ngeli ya A_WA**

Kijana **alichora** picha ya kuvutia

Vijana **walichora** picha za kuvutia

Mlanguzi **atachukuliwa** hatua Kali

Walanguzi **watachukuliwa** hatua Kali

**Nomino za ngeli ya U_I**

Tambua nomino za ngeli ya U_I katika mraba ya maneno ufuatao.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | T | A | R | O | O | M |
| K | S | D | E | A | V | K |
| E | B | M | U | W | A | O |
| B | M | K | U | K | I | N |
| E | T | K | U | K | I | O |
| H | A | I | M | T | I | D |
| C | A | J | P | T | E | B |
| M | L | A | N | G | O | S |

Nomino za ngeli ya U_I kwenye jedwali ni:-

Mkebe

Mtaro

Mkuki

Mlango

Mkono

**Viambishi vya ngeli ya U_I**

Mkebe **una** maji

Mikebe **Ina** maji

Mlango **umefungwa**

Milango **imefungwa**

Mfuko **umenunuliwa**

Miduko **imenunuliwa**

**MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA MAWASILIANO**


**KUSIKILIZA kwa kina**

<u>Sauti d na nd katika silabi ya maneno</u>

do, da, di, du, de

ndi, ndu, nde, nda, ndo

Chati ya maneno



**KUSOMA**

**KUSOMA UFAHAMU**

1.(*a*) **Soma kifungu kifuatacho**:

Tawa alizaliwa na kulelewa na wazazi wake kule Kita. Alijiunga na shule ya msingi huko huko. Tawa alikuwa na bidii za mchwa. Msukumo huu wa ndani kwa ndani ulitawala na kuelekeza maisha yake. Shuleni alikuwa mwepesi darasani. Si hivyo tu, alikuwa pia mwepesi wa kusaidia wenzake. Alijifunza maadili kutoka kwa walezi wake. Hili lilifanya apendwe na walimu pamoja na wanafunzi wenzake. Alikuwa na mlahaka mwema na kila aliyehusiana naye.

Siku moja wakati wa likizo ya muhula wa pili, Tawa alitumwa na mzazi wake kununua bidhaa sokoni. Alipokuwa anakaribia soko, aliona gari kubwa jeusi limeegeshwa kando ya barabara. Ndani kulikuwa na watu ambao walikuwa na darubini mikononi. Kila mmoja alikuwa na darubini yake ambayo ilielekezwa kwenye boma la mkazi mmoja aliyeitwa Haji. Tawa alishtuka na kusimama. Alikita macho walipokuwa. Alijificha ili asionekane. Miguu ikawa mizito. Alihisi joto na baridi kwa wakati mmoja.

**Maswali ya ufahamu**

I. Nini kiliwasaidia polisi kuwanasa majangili? Jibu: kamera za Siri.
II. Majangili walielekeza darubini zao wapi? Jibu: kwenye boma la Haji.
III. Jadilini sifa za Tawa jinsi zinavyojitokeza kwenye kifungu? Jibu: Tawa alikuwa mwenye Bidii, alikuwa mwerevu,alikuwa mwepesi wa kusaidia na pia alikuwa jasiri alipowasaidia polisi kuwakamata majangili
IV. Gari LA majangili lilikuwa la rangi gani? Jibu: jeusi

2. Jadili na mwenzako mambo yanayokuongoza kudondoa habari mahususi katika kifu. Jibu: ujumbe katika Kila Aya hukusaidia kudondoa habari ya kifungu.

'Lazima hapa pana tatizo!' alijiambia. Aliwaza na kuwazua. Alijiuliza maswali mengi kimoyomoyo. "Hawa ni kina nani? Mbona wana darubini? Wanaangalia nini kwa Haji? Ikiwa ni wageni wake mbona wasiende langoni wafunguliwe? Mbona gari limeegeshwa mbali upande ule mwingine? Nivunje safari au niendelee?" Tawa alipiga moyo konde na kuamua kuendelea na safari yake. Ujasiri fulani ukamwingia. Akapata nguvu mpya za kuendelea na safari.

Kabla ya kuondoka alichukua nambari ya usajili ya gari la watu hao. Alipita kwa kasi mahali hapo. Alielekea katika KITUO CHA POLISI CHA MAVUNO. Alikata kauli kwenda kuripoti yale ambayo aliyaona. Aliwaambia askari alishuku matendo ya waliokuwemo garini. Aliwapa nambari ya usajili wa gari hilo.

Askari hawakusita. Waliondoka mara moja kwenda kuwanasa majangili hao. Walipokaribia, majangili waliondoka kwa gari lao kwa kasi. Muda si muda ving'ora vilisikika hewani. Mlio wa ving'ora uliwavutia wanakijiji mahali hapo. Haji pia alifika hapo. Haji aliwatuliza wanakijiji ambao walikuwa wameghadhabishwa na kutoroka kwa majangili hao.

"Tulieni, tulieni, tulieni jamani! Msiwe na wasiwasi. Hapa kwangu nimeweka kamera za siri. Nina hakika kamera hizo zimewanasa watu hao waliokuwa hapa. Polisi watazikagua na kuzitumia kuwasaka."

Mkuu wa polisi aliyekuwepo alisema, "Wananchi msiwe na hasira. Ningependa kumpongeza Haji kwa kuziweka kamera za siri. Ninawaahidi kuwa teknolojia hii ni njia moja ya kulinda usalama wetu. Bila shaka watu hao watapatikana."

Uchunguzi wa polisi kupitia kamera za siri uliwawezesha kutambua na hatimaye kuwanasa watu hao.

3. Dondoeni maneno mageni yaliyotumika katika kifungu.

- Bidii za mchwa _ kuwa na Bidii sana
- Mwepesi darasani_ kuwa mwerevu
- Darubini_ kifaa kinachoonesha vitu kwa mbali
- Pigia Moyo konde_ kuamua
- Pita kwa kasi_ tembea haraka
- Ving'ora_ sauti inayoonyeaha kutoka kwa jambo au Kuna hatari
- Kamera za siri_ kifaa Cha kidigotali kinachorekodi matokeo yanayotokea bila yeyote kujua.

**KUANDIKA**

**Insha ya KUBUNI**

<u>Vipengele vinavyozongatiwa kujenga wazo katika insha.</u>

- Utangulizi
- Mwili
- Itimisho
- Mada inayozungumziwa

**Mfano wa insha ya masimulizi**

NGIRI NA WANAWE

Hapo zamani za kale paliondokea Ngiri na wanawe. Walipenda kula matunda ya mwituni yaliyoiva. Hata hivyo, tatizo kubwa lilikuwa namna ya kuyapata matunda hayo. Ngiri aliwaza na kuwazua ili apate utatuzi wa tatizo hilo.

Siku moja Ngiri na wanawe walimuona Ndovu na wanawe wakila maembe yaliyoiva kwa furaha. Ngiri alikwenda kumuuliza Ndovu siri ya kuangua matunda

yaliyoiva. Ndovu alisema, "Ndugu yangu, kuangua matunda ni rahisi sana. Mimi hushika shina la mti kwa mkonga wangu kisha hutingisha kidogo tu. Kusudi ni kuhakikisha tu nimeangua matunda kiasi yaliyoiva. Wajua lazima nihakikishe kuwa siangui matunda yote. Kuna leo na kuna kesho eti!" "Aah! Kumbe ni rahisi hivyo! Laiti ningekuwa na mkonga, pia ningewaangulia wanangu matunda." Ngiri alisema. "Huna mkonga lakini una akili. Akili ni mali itumie." Ndovu alimshauri Ngiri. Ndovu alimkaribisha Ngiri na wanawe kula maembe hadi shibe yao.

Ngiri na wanawe walimshukuru Ndovu na kwenda zao. Siku iliyofuata Ngiri aliuona mpera uliokuwa na mapera yaliyoiva. Alikumbuka nasaha za Ndovu. Alikimbia mbio na kugonga shina la mpera kwa kichwa chake. Mpera ulitingika na mapera yaliyoiva yakaanguka. Kwa bahati mbaya meno ya Ngiri yalikwama kwenye shina la mpera. Kumbe alikuwa amesahau kufunga kinywa alipogonga shina la mpera.

Ngiri alianza kujivuta kutoka kwenye shina la mpera huku akisaidiwa na wanawe. Kadri alivyoendelea kujivuta ndivyo meno yake yalivyoendelea kurefuka. Mwishowe Ngiri alijinasua lakini meno yake mawili ya kando yalichomoka na kuwa marefu kama pembe. Ngiri alifurahi kuwa alivumbua mbinu ya kuangulia wanawe matunda. Siku hiyo wanawe walikula mapera kwa furaha. Baadaye Ngiri aligundua kuwa pembe zake mpya zingemsaidia kupambana na adui. Alienda kwa Ndovu kumshukuru kwa ushauri wake mzuri.


**Maswali:**

Andika insha ya masimulizi kuhusu **Safari ya ajabu.**

**SARUFI**

**Ngeli ya ki_ vi**

Vitu vilivyo katika ngeli ya ki- vi



**Viambishi vya ngeli ya ki-vi katika sentensi**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (i) | Kifutio kilitumika kufuta maandishi. | Vifutio vilitumika kufuta maandishi. |
| (ii) | Kipakatalishi kitatumiwa kuhifadhi kazi ya mwanafunzi. | Vipakatalishi vitatumiwa kuhifadhi kazi za wanafunzi. |
| (iii) | Chumba cha mgeni kinafagiliwa. | Vyumba vya wageni vinafagiliwa. |
| (iv) | Kisa alichosimulia kilimvutia mwanafunzi. | Visa walivyosimulia viliwavutia wanafunzi. |
| (v) | Chombo cha mawasiliano kitanunuliwa. | Vyombo vya mawasiliano vitanunuliwa. |

**Tunga sentensi katika umoja na wingi ukitumia nomino zifuatazo:**

Kibanio_

Kizingiti_

Kiambaza

Cheo_

Cherehani_

**Ngeli ya Li- Ya**

<u>Maneno katika ngeli ya Li-Ya ni majina ya sehemu za mwili,matunda na vitu vingenevyo.</u>

Mfano za nomino katika ngeli ya Li-Ya

| | |
|---|---|
| jiwe | mawe |
| tawi | matawi |
| kilima | vilima |
| jina | majina |
| uovu | maovu |
| jembe | majembe |
| neno | maneno |
| ziwa | maziwa |
| jicho | macho |
| tunda | matunda |

**Viambishi vya ngeli ya Li-Ya kwenye sentensi:**

1. (a) Soma sentensi zifuatazo:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | Tingatinga linatumia teknolojia ya kisasa kuvuna mpunga. | Matingatinga yanatumia teknolojia ya kisasa kuvuna mipunga. |
| (b) | Sikio lake limetibiwa. | Masikio yao yametibiwa. |
| (c) | Jibu lilisomeka vizuri kwenye kiwambo cha simu. | Majibu yalisomeka vizuri kwenye viwambo vya simu. |
| (d) | Gari litafungwa mlango kwa kiungambali. | Magari yatafungwa milango kwa viungambali. |
| (e) | Duka liliwekwa kamera ya siri. | Maduka yaliwekwa kamera za siri. |

Tunga sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia nomino zifuatazo:

I) Shamba
II) Soko
III) Ua
IV) Jokofu
V) Tawi

**Nyimbo za KAZI**

Nyimbo za KAZI huimbwa WAKATI wa kufanya KAZI au kuwahimiza watu wapende KAZI

**Mifano za wimbo za KAZI**

*Uzembe ndio hasimu wa ujenzi wa nchi,*
*Kwa kuwa ndio sababu hasa chanzo cha njaa.*
*Ewe mwenzi wangu kumepambazuka,*
*Chukua jembe na uma tukalime.*
*Pia wewe dereva kumepambazuka,*
*Huu ndio muda wako, wa kwenda kazi.*

*Uzembe,*
*Ndiye hasimu wa kujenga nchi,*
*Tujitenge, na uzembe tuijenge nchi.*


*Mwenzi wangu,*
*Kumekucha toka twende shamba,*
*Tujitenge, na uzembe tuijenge nchi.*

*Askari wee*
*Kumekucha kashike doria,*
*Tujitenge, na uzembe tuilinde nchi.*

**Ujumbe katika wimbo huu hapo chini ni kwamba:-** watu wafanye KAZI waache uzembe, kwani uzembe huleta njaa na pia huharibu nchi

**Wimbo kama hii huimbwa kwa Nini?** Wimbo huu huimbwa kuwahimiza watu kufanya KAZI kwa bidii ili tujenge nchi yetu.

**Mazingira ambamo nyimbo za KAZI huimbwa**



Mimi hapa ni mwalimu × 2
Niko ndani ya darasa × 2
Nitakupa kitabu kizuri,
Mwanafunzi soma kwa furaha.

Na mimi ni daktari × 2
Niko hapa hospitali × 2
Ninatibu wagonjwa vizuri,
Mwanafunzi soma kwa furaha.

Mimi nami ni mchuuzi × 2
Nimefika sokoni mapema × 2
Nauza matunda mazuri,
Maembe, ndizi hata na mapera.


**Taja wafanyakazi wanaozungumziwa katika wimbo huu:-** mwalimu, daktari,mchuuzi.

**Elezeni mahali pa KAZI palipotajwa:-** darasa, hospitali,sokoni

**Nyimbo za dini**

Nyimbo za dini huimbwa WAKATI wa kumtukuza mungu na huimbwa kanisani.

<u>Mfano wa nyimbo za dini</u>


Mungu yu mwema,
Mungu yu mwema,
Mungu yu mwema,
Yu mwema kwetu.

Yu mwema ametubariki,
Yu mwema ametushibisha,
Yu mwema ametupa nguvu,
Yu mwema kwetu.

**Ujumbe katika wimbo huu ni kwamba:-** mungu ni mwema,ametubariki,ametushibisha,ametupa nguvu.

**Wimbo huu huimbwa kwa nini:-** ili kumtukuza mungu.

**Kusoma KWA kina_ wahusika**

<u>Wahusika katika novela ya chozi la heri.</u>

**Ridaha_** anavumilia matukio yaliyomkumba kijijini mwake kama vile kufukuzwa na Mali yake kuharibika.

Ridhaa ana uwezo wa kuhisi kuwa janga lisilo la kupendeza litaifikia familia yake.

- Ridha ni mwenye bidii za mchwa
- Ni mvumilivu
- Mwenye busara

**Terry** – Ni mke wa ridhaa

<u>Sifa zake</u>

<u>Mcheshi.</u> Ucheshi ulikuwa ni mazoea yake ya kawaida

<u>Mwenye busara</u> – Anajaribu kumpa ushauri mumewebbaada ya kumwona mumewe kama mshirikina .

**Wahusika** ni viumbe ambavyo hutumika na mwandishi katika kazi za fasihi. Wahusika wanaweza kuwa watu,vitu au wanyama.

**Kuandika**

<u>Barua ya kuomba msamaha</u>

Barua ya kuomba msamaha huandikwa jinsi unavyoandika barua rasmi


Unaweza kuandika barua ya kuomba msamaha kuhusu

- kukosa shuleni
- Kukosa kufanya KAZI ya mwalimu
- Kuvunja Sheria ya shule

Mambo muhimu ya kuzingatia unapoandika barua ya kuomba msamaha ni :

- Anwani Huwa mbili, ya mwandikiwa na ya anayeandikiwa
- Andika kile ambacho barua inahusu
- Andika sababu ya wewe kuomba msamaha
- Andika sahihi mwishoni mkono wa kushoto

Mfano wa insha ya kuomba msamaha



Shule ya Msingi ya Jiimarishe,
S.L.P. 03246-001,
MASOMONI.
11.01.2023

Bi. Zuru,
Shule ya Msingi ya Mlindeni,
S.L.P. 04326-001,
MASOMONI.

Kwa mwalimu wangu wa Gredi ya Saba,

KUH: KUKOSA KUHUDHURIA SHULE WIKI HII

Naandika barua hii ili kukuomba radhi. Samahani sikukujuza mapema kuwa sitaweza kuhudhuria shule wiki hii. Nimelazwa hospitalini baada ya kuumia mguu wakati wa wikendi nilipokuwa nikicheza.

Naomba uwaruhusu wenzangu katika kikundi chetu kuwasilisha mradi wangu kwa niaba yangu. Nakusihi pia unitumie kazi ya mazoezi kwa njia ya kidijitali nifanyie huku hospitalini nikiweza. Tafadhali tumia anwani ya baruapepe ya mzazi wangu chema442@gmail.com.

Nikimalizia, nakuomba uwajuze wenzangu kuhusu ajali hii iliyonifika. Wasalimie wote. Tutaonana wiki ijayo majaliwa.

Wako mwaminifu,

Moris Juma Kinabwa.

Zoezi

Umechelewa kurudi darasani baada ya kupewa ruhusa. Mwalimu wako amekuambia uandike barua rasmi ya kuomba msamaha. Andaa vidokezo vya barua rasmi ya kuomba msamaha utakayoandika.

Vidokezo:

1. Barua inahusu Nini
2. Kwa Nini ulichelewa

3. Nini kilitendeka
4. Nini kilisababisha wewe kuchelewa kurudi darasani.

Andika barua rasmi ya kuomba msamaha kwa kuzingatia ujumbe,muundo na lugha ifaayo. Rejelea vidokezo ulivyoandika ili kukuelekeza.

Shule ya msingi ya soy

S L P 1295

Eldoret

25-10-2023

Bw Nyongesa

Shule ya msingi ya soy

S L P 29

Eldoret

Kwa mwalimu wangu wa darasa ,

KUH: KUCHELEWA KURUDI DARASANI BAADA YA KUPEWA RUHUSA

Naandika barua hii ili kukuomba radhi kwa kuchelewa kurudi darasani baada ya kupewa ruhusa. Samahani kwa sababu baada ya Mimi kukuomba ruhusa na kuelekea msalani,nilimkuta mwanafunzi wa gredi ya kwanza pale nje uwanjani ambaye hakuwa anajihisi vizuri. Nilipata mwanafunzi huyo akitapika uwanjani huku akionekana mnyonge sana. Nilichukua jukumu ya kumsaidia maana hakukuwa na mwingine wa kumsaidia

Nilichukua mwanafunzi huyo na kumpeleka kwenye kituo Cha matibabu ili atibiwe, na hii ndio sababu ilionifanya Mimi kuchelewa kurudi darasani.Tulipomaliza matibabu niliwajulisha wazazi wake ili waje kumpeleka nyumbani akapumzike.

Natumai mwalimu utazingatia ombi langu na kuniruhusu kuendelea na masomo yangu

Wako mwaminifu

D J

Deborah Jebet

**SARUFI**

Vinyume vya maneno

Vinyume ni maneno yenye maana yanayopingana na maana ya neno linguine ,mfano:

Usiku_ mchana

Furahi_ huzuni

Lia _ Cheka

Pika_ pakua

Njaa_ shibe

Giza _ mwangaza

**Pigia mstari nomino na kinyume chake katika Kila fungu la maneno.**

a) Ana ujasiri,aliwakomesha mafisadi wenye uoga
b) Hivyo basi , huzuni hutokea Hali ikikosekana nayo furaha huja haki ikipatikana.
c) Talanta yake ilimpa faida,akaepuka hasara ya kupotezs muda wake kwa kuketi tu.
d) Mwenye shibe hamjui mwenye njaa

Sungura alijidai mwerevu. Aliwaona wanyama wenzake kuwa wajinga sana. Hakujua kuwa pwagu anaweza kupata pwaguzi. Sungura alianzisha biashara ya kuwekea wanyama pesa benkini. Kobe alikuja kuweka pesa zake. Baada ya muda Kobe aliendа kutoa hela kidogo. Sungura alimkataza Kobe kutoa pesa kidogo.

Alisema,"Huwezi kutoa hela chache hivyo. Hatutaki maskini. Hii ni benki ya matajiri," Sungura alisema kwa ukali.

"Sawa. Wacha ukali. Upole utakufaa. Sipendi ubishi. Nitatoa pesa zangu zote. Naomba unihesabie," Kobe alisema kwa unyenyekevu.

Sungura aliangalia akaunti ya Kobe. Alishangaa kuona kuwa Kobe alikuwa na mabilioni ya pesa. Alianza kumuomba Kobe msamaha kwa ujeuri wake.

"Usinione hivi. Najiamini na kujithamini ndugu yangu. Uvumilivu wangu umekupa funzo," Kobe alimwambia Sungura kwa upole kisha akaondoka.

**Soma kifungu hiki Cha hadithi**

**Maswali:**

1. Tambueni nomino zilizo na vinyume vyake katika kifungu ulichosoma

- Mwerevu_ mninga
- Pwagu_ pwaguzi
- Weka_ toa
- Maskini_ tajiri
- Ukali_ upole

**Jaza nafasi zilizoachwa kwa kinyume Cha neno lililokolezwa rangi.**

a) Baada ya **dhiki** faraja
b) Umoja ni **nguvu,**utengano ni udhaifu
c) Mtahini na **mtahiniwa** njia Yao ni moja.
d) Lililo na **mwanzo** halikosi mwisho
e) Mwenda **pole** na omo marejeo ni ngamani

**Tunga sentensi ukitumia vinyume vya nomino hizi**

a) Baraka_ Baba alitoa laana kwa mtoto wake
b) Utamu_ Tunda like lilikuwa na ukali
c) Raha_ Familia iliishi kwa shida sana
d) Wema _ Ubaya wake ulimuletea hasara
e) Baridi_ Lilikuwa na joto nyingi sana

**Vinyume vya vivumishi**

<u>Neno na kinyume chake</u>

Jasiri_ mwoga

Tamu_ chungu

Haramu_ halali

Mwema_ mui

Polepole_ haraka

Pigia mstari kivumishi na kinyume chake kwenye Kila fungu la maneno yafuatayo

1. Nyumba <u>ndogo</u> imejengea kando ya nyumba <u>kubwa</u>
2. Nguo yangu Ina madoa <u>meupe</u> na <u>meusi</u>
3. Mshipi <u>mrefu</u> umekatika lakini Ile <u>mfupi</u> uko sawa
4. Viti <u>vichache</u> vimepangwa, <u>vingi</u> Bado viko mbele ya lango

**Zoezi la wanafunzi**

Tunga kifungu Cha maneno kwa kutumia vinyume vya vivumishi hivi:

a) ZZito
b) Rahisi
c) -embamba
d) Zu-ri
e) -ingi

**11: MAJUKUMU YA WATOTO**

**Kuzungumza kwa kuambatanisha vitendo na ishara**

MAWASILIANO kwa kutumia maneno na vitendo Huwa tunasrma anazungumza kwa kuambatanisha vitendo na ishara.

**Mifano za vitendo na ishara katika mazungumzo ya Kila siku**

Enda

Kuja

Kimbia

Keti

Pika

Kwaheri

Lala

Lima

Ongea

**Kusoma**

**Kusoma KWA mapana**

Matini ni kitu chochote ambacho husomwa na kutoa ujumbe katika jamii

Chagua kitabu chochote unachopenda kusoma ,Kisha baada ya kusoma kitabu hicho:

a) Eleza kichwa Cha nakala uliosoma
b) Eleza ujumbe unaonitokeza kwenye nakala
c) Taja msamiati uliotumika kwenye nakala
d) Tunga sentensi ukitumia msamiati kutoka kwenye nakala
e) Andika muhtasari wa nakala uliosoma
f) Weka rekodi ya matini uliyosoma

**KUANDIKA**

**Insha za KUBUNI _ maelezo**

Mambo ya kuzingatiwa unapoandika insha ya matini:

- Kichwa
- Utangulizi
- Ujumbe
- Hati nadhifu
- SARUFI sahihi.
- Mtiririko ufaao wa maelezo
- Muundo wa mtindo ufaao
- Msamiati na tahajia sahihi.

Mfano wa insha ya maelezo:

## MAJUKUMU YA WATOTO

Watoto wana majukumu mengi muhimu. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya, mtoto ni mtu aliye na miaka chini ya kumi na minane.

Jukumu kubwa na muhimu kwa kila mtoto ni kusoma ili kujipatia elimu. Elimu itamwezesha kupata maarifa, stadi na mitazamo ifaayo maishani. Kwa hivyo, mtoto hana budi kuwajibika shuleni huku akikumbuka kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame. Anahitajika kusoma kwa makini ili kupata umilisi unaotarajiwa. Aidha, pale anapopata changamoto, anaweza kuelekezwa na mwalimu. Wakati wote, mtoto anashauriwa kudumisha nidhamu.

Vilevile, ni jukumu la watoto kujitunza. Jukumu la kujitunza hujumuisha kunawa, kuoga, kufua na kuvaa nguo safi. Mtoto anayewajibika pia, hutunza mazingira yake shuleni na nyumbani.

Isitoshe, watoto wana jukumu la kuwatii na kuwasaidia wazazi na walezi wao nyumbani. Hii huwa pia ni fursa nzuri kwa mtoto kujifunza kazi za nyumbani, shambani na nyinginezo katika mazingira anamoishi.

Kila mtoto anafaa kutimiza majukumu yake kwa bidii. Mtoto ana wajibu wa kuchagua marafiki waadilifu. Sharti aepuke hali na mazingira ambayo yanaweza kuvuruga na kudhuru akili yake. Haya yote yatamsaidia kukua akiwa mtu muungwana.

**SARUFI**

**<u>Mnyambuliko wa vitenzi</u>**

Mnyambuliko wa vitenzi ni jinsi vitendo vinavyobadilika kutegemea kauli mbalimbali. Mfano ni kitenzi **osha** kimebadilika na kuwa **Oshea** na **Oshwa**

**Kauli ya kutenda** ni maneno katika Hali yake ya kawaida mfano: osha,soma,Lima,imba, pika.

**Matumizi ya vitenzi katika kauli ya kutenda**

Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo:

a) Futa- mwanafunzi alifuta ubao
b) Osha- mama aliosha nguo
c) Vua- mvuvi alivua samaki
d) Fua- msichana alifuta nguo zake
e) Tembea- tulitembea Hadi shuleni Jana
f) Choma- baba alichoma takataka baada ya kusanya.

**Kauli ya kutendea**

- Vitenzi katika kauli ya kutendea huishia kwa -ia, -ea na WAKATI mwingine – Lia na lea. Kwa mfano: safishia,O'Shea,fungulia na tembelea.
- Kauli ya kutendea huonyesha Hali ya kufanya kitendo:

i) Kwa Niaba ya mwingine k.m. Nilimwoshea mama vyombo
j) Kwa kutumia kifaa Fulani k.m. Nilitumia sabuni kuoshea vyombo
k) Kwa ajili ya mwingine k.m. Nilimfungulis mgeni mlango aingie

**Zoezi**

**Panga maneno ili kutunga sentensi sahihi**

a) Mkeka aliwatandikia wageni yangu dada juzi.

Jibu: Dada yangu aliwatandikia wageni mkeka juzi

b) Mbuga tulitembelea uliopita muhula za wanyama pori.

Jibu: Tulitembelea mbuga za wanyama muhula uliopita.

c) Aliwapikia mpishi kitamu wageni chakula.

Jibu: Mpishi aliwapikia wageni chakula kitamu

d) Nitamwandikia kwa simu ujumbe mfupi baba

Jibu: Nitamwandikia baba ujumbe mfupi kwa simu.

e) Kiti ili abiria waketi alimsongea pamoja

Jibu; Abiria walimsongea kiti ili waketi pamoja.

f) Mgonjwa alimlipia dawa yangu kaka

Jibu: Kaka yangu alimlipia mgonjwa dawa.

**Kauli ya kutendwa**

Vitenzi katika kauli ya kutendwa huonyesha Hali ya kuathirika kutokana na kitendo au kufanywa kwa kitendo k.m mlango umefungwa.

**Mfano wa maneno katika Hali ya kutendwa:**

Fungwa,imbwa,jazwa,pakwa,pendwa,ponywa,takaswa,pelekwa.

**Zoezi**

**Geuza sentensi hizi ziwe katika hali ya kutendwa**

a) Mama amepika chakula. Jibu: Chakula kimepikwa na mama.
b) Mwalimu amefunga mlango. Jibu: mlango umefungwa na mwalimu
c) Akinyi ameandika ujumbe. Jibu: ujumbe umeandikwa na akinyi
d) Mogambi alitandika kitanda. Jibu; kitanda kilitandikwa na Akinyi.
e) Dereva aliendesha gari. Jibu: gari liliendeshwa na dereva

**Zoezi la mwanafunzi**

**Kamilisha sentensi kwa kugeuza kitenzi kilicho kwenye mabano kiwe katika kauli ya kutendwa**

a) MAJUKUMU yote yali________ ifaavyo(tekeleza)
b) Keki ili_______ vizuri san(oka)
c) Mwizi aliye______ amepelekwa mahakamani ( shika)
d) Makosa yaliyo_______ yamerekebishwa( fanya)
e) Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uli______ katika Sherehe (imba).